**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**614** **MAARIFA YA JAMII**

**Muda: Saa 3.** **Mwaka: 2009**

---

**Maelekezo.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu **B** na **C.**
3. Zingatia maelekezo ya kila swali.
4. Andika majibu yako kwa kalamu ya wino wa bluu au mweusi isipokuwa michoro ambayo itachorwa kwa penseli.
5. Vikokotozi **haviruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
6. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
7. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. (a) Eleza maana ya kipimo cha ramani.

   (b) Bainisha aina mbili za ramani.

   (c) Taja aina tatu za ramani kulingana na matumizi yake.

2. (a) Eleza kwa kifupi dhana ya kanda za masaa.

   (b) Kama katika mji wa Freetown 15° Magharibi ni saa 11:00 alfajiri, kokotoa muda katika mji wa Morogoro 35° Mashariki.

   (c) Mji wa Dar es Salaam upo kwenye longitudo 39° Mashariki. Ikiwa ni saa 12:00 mchana huko Morogoro 35° Mashariki, ni saa ngapi Dar es Salaam?

3. (a) Bainisha mizunguko ya Dunia kisha fafanua athari za kila mzunguko.

   (b) Bainisha matokeo yanayoweza kutokana na mzunguko wa mwezi kuzunguka dunia.

4. Tofautisha mistari ya kontua kuonesha maumbile yafuatayo:

   (a) Pitiyo

   (b) Genge

   (c) Kigongo

   (d) Uwanda wa juu

5. Eleza tofauti kati ya **Zinjanthropus** na **Homo habilis** kama hatua muhimu katika mabadiliko ya kimaumbile kwa binadamu.

6. Bainisha mambo manne yaliyokuwa chanzo cha migogoro ya kisiasa katika nchi za Kiafrika baada ya uhuru.

7. Taja sababu kuu nne zilizofanya watawala wa jadi katika Bara la Afrika kushindwa kupinga uvamizi wa kikoloni kutoka Bara la Ulaya mwishoni mwa karne ya 19.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

8. Kwa kutumia mifano miwili eleza namna kila aina ya milima ifuatayo inavyotokea:
   (a) Milima mikunjo
   (b) Milima ya tofali
   (c) Milima ya volkano

9. (a) Eleza kwa kifupi dhana ya ukoloni.
   (b) Toa mifano miwili ya nchi zilizotawaliwa na Uingereza, Ujerumani, Ureno, Ubelgiji na Ufaransa katika nusu ya pili ya karne ya 19.

10. Bainisha sababu nne zilizochangia wafanyabiashara wa karne ya 19 kutoka Ulaya kujishughulisha na bidhaa za kilimo na malighafi kwa ajili ya viwanda vya Ulaya.

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu swali moja (1) kutoka katika kila kipengele.

### Kipengele I: Jiografia

11. Kwa kutumia mifano ya nchi za Afrika Mashariki na Kati bainisha njia nne za kudhibiti upotevu wa vyanzo vya maji.

12. Bainisha hatua tano zinazoweza kuchukuliwa katika juhudi za kupunguza athari za uharibifu wa misitu kama vile mmomonyoko wa udongo na ukame.

### Kipengele II: Historia

13. Chambua mambo matano yaliyotokea katika mataifa ya nje ambayo yaliongoza katika harakati za kudai uhuru katika Bara la Afrika.

14. Tambua sababu tano zilizopelekea kuongezeka kwa biashara ya Afrika Mashariki na Ulaya.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU C (Alama 30)

Jibu swali **moja (1)** kutoka katika kila kipengele.

### Kipengele I: Jiografia

15. Kutokuwepo kwa nidhamu miongoni mwa wanafunzi katika darasa la Jiografia kumeathiri ufundishaji wa somo hili. Fafanua hoja hii.

16. Ainisha mambo matano ambayo mwalimu anatakiwa kuangalia wakati wa kutumia kazimradi kama njia ya kufundishia na kujifunzia somo la Jiografia.

### Kipengele II: Historia

17. Mwalimu mwenye uzoefu katika ufundishaji wa somo la Historia hahitaji kuwa na miongozo ya ufundishaji. Eleza hoja hii.

18. Fafanua faida tano za matumizi ya shajara katika kufundishia na kujifunzia somo la Historia.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org